

HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA

SIMU: MKURUGENZI WA MANISPAA

+ 255 736 200910

OFISI ZOTE: +255 736 200911/12

FAX: +255 028 736 200910

Barua pepe: md@ilemelamc.go.tz

Tovuti:www.ilemelamc.go.tz

Ofisi ya Mkurugenzi,

Manispaa ya Ilemela,

S.L.P 735,

MWANZA.

TAARIFA KWA UMMA

Mkurugenzi wa Manispaa ya Ilemela, John Paul Wanga amemfikisha Bi Bertha Fabian kituo cha polisi kwa kosa la kuidanganya Serikali kwa nyaraka za kughushi vyeti na barua ya Katibu Mkuu Utumishi.

Amechukua hatua hiyo ya kumshikilia Bi Bertha Fabian na kumfikisha kituo cha polisi ili akaisaidie polisi kufahamu ni wapi na akina nani waliomtayarishia cheti cha ualimu, cheti cha kidato cha nne na barua ya Katibu Mkuu Utumishi baada ya kufika ofisi ya utumishi ili aweze kurudishwa katika mfumo wa malipo ya mshahara.

Bi Bertha ambaye ni mwalimu katika shule ya msingi ya Buzuruga alifika ofisi ya utumishi huku akiwa na vyeti vya shule pamoja na barua kutoka kwa Katibu Mkuu Utumishi vilivyoonekana kuwa ni vya kughushi huku akidai kuwa ameagizwa kwa Mkurugenzi amrudishe katika mfumo wa malipo ya mshahara.

“Sijaona barua yoyote kutoka kwa katibu wa baraza la mitihani inayoniambia mimi Mkurugenzi kuwa tumepitia kumbukumbu zetu na tumeridhika kuwa Mwalimu huyo ni mhitimu halali”, alisema Mkurugenzi

Mtumishi huyo alibainika kutokuwa na sifa ya kuendelea kuwa mtumishi wa umma kutokana na kuwa na vyeti feki baada ya zoezi la uhakiki wa vyeti kwa watumishi liliondeshwa nchi nzima na hivyo kusimamishiwa mshahara wake.

Katika zoezi hilo watumishi wote waliobainika kuwa na vyeti feki waliondolewa kwenye Utumishi na kusimamishiwa mshahara jambo ambalo bi Bertha ilikuwa ngumu kukubaliana nalo.

Afisa Utumishi Bi Jane Malongo alisema kuwa Bi Bertha hakukubaliana na hatua hiyo iliyochukuliwa dhidi yake na hivyo kukata rufaa. Aliongeza kuwa mnamo tarehe 15/02/2018 Bi Bertha alifika ofisi ya utumishi Ilemela akiwa na cheti cha taaluma akidai kuwa amepewa na baraza la mitihani pamoja na barua kutoka kwa Katibu Mkuu Utumishi iliyokuwa ikimuelekeza Mkurugenzi kumrudisha mtumishi huyo katika mfumo wa malipo ya mshahara.

“Baada ya kuipitia barua na cheti alichowasilisha nilibaini kuwa nyaraka hizo ni za kughushi” Na hivyo niliamua kumuweka chini ya ulinzi wa mgambo wa ofisini huku nikisubiri hatua zaidi kutoka kwa mkurugenzi” alisema bi Jane Mallongo.

Kufuatia kosa hilo la Bi Bertha, Mkurugenzi wa Manispaa ya Ilemela ametoa rai kwa watumishi wote ambao walibainika na kuondolewa katika utumishi baada ya zoezi la uhakiki wa vyeti feki kuacha mara moja tabia ya kughushi nyaraka mbalimbali za kiserikali ili kurejeshwa kazini kwani kwa kufanya hivyo ni kuendelea kufanya makosa na hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yao.

Imetolewa na Kitengo cha Tehama, Habari,Uhusiano na Mawasiliano

Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela

15/02/2018